# JUMUIYA YA TAWALA ZA MITAA TANZANIA

# (ALAT)

## Mradi wa Uboreshaji Mazingira ya Biashara (LIC)



## Uzoefu wa Uwekezaji Kutoka Mradi wa Umwagiliaji: Skimu ya Umwagiliaji Titye, Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, Mkoa wa Kigoma, Tanzania

# Uzoefu Kutoka katika Uwekezaji wa Mradi wa Umwagiliaji

# Mfano Kutoka katika Ukarabati wa Skimu ya Titye

# Iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, Mkoa wa Kigoma Tanzania

Ripoti ya Mradi imeandaliwa
na

**Jumuiya ya Tawala za Mitaa (ALAT),**
**S.L.P. 2049,**
**DODOMA**

Imefadhiliwa na

**Mradi wa Uboreshaji Mazingira ya Biashara (LIC)**

Kwa kushirikiana na

**Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu**
**Agosti, 2018**

## YALIYOMO


**SHUKRANI ...... ii**
**UTANGULIZI ...... iii**
**VIFUPISHO ...... iv**
**SURA YA KWANZA ...... 1**
**UTANGULIZI ...... 1**
1.0. Usuli ...... 1
1.1. Idadi ya Wakazi wa Wilaya ya Kasulu ...... 3
1.2. Tatizo la Utafiti ...... 3
1.3. Eneo la Mradi ...... 5
1.4. Malengo ...... 6
1.4.1. Lengo Kuu ...... 6
1.4.2. Malengo Mahususi ...... 6
1.5. Eneo la Mradi ...... 6
**SURA YA PILI ...... 7**
**UFUMBUZI WA MATATIZO ...... 7**
2.1 Mfereji wa Umwagiliaji ...... 7
2.2 Uendeshaji na Ukarabati ...... 7
2.3 Usambazaji wa Maji na Mifumo ya Udhibiti ...... 7
2.4 Uwezeshaji wa Wakulima na Shughuli Nyingine katika Mradi ...... 8
2.5 Usimamizi wa Kazi ...... 8
**SURA YA TATU ...... 9**
**UTEKELEZAJI, MPANGILIO NA MATOKEO/ MATARAJIO YA MRADI ...... 9**
3.1 Utekelezaji na Majukumu Yao ...... 9
3.2 Ushiriki wa LIC na Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu Kwenye Mradi wa Umwagiliaji wa Titye ...... 9
3.3 Matarajio ya Mradi ...... 10
3.3.1 Kuongeza Uzalishaji wa Mazao, Kipato cha Mkulima na Kupunguza Umasikini ...... 10
3.3.2 Uimarishaji Matumizi ya Maji katika Skimu ...... 10
3.3.3 Kuwajengea Uwezo Jumuiya ya Umwagiliaji ...... 11
**SURA YA NNE ...... 12**
**GHARAMA NA UPATIKANAJI WA FEDHA ZA KUENDESHA MRADI ...... 12**
4.1 Gharama za Mradi ...... 12
4.2 Muda wa Utekelezaji wa Mradi ...... 12
**SURA YA TANO ...... 13**
**CHANGAMOTO, VIKWAZO NA UIMARA WA MRADI ...... 13**
5.0 Changamoto ...... 13
5.1 Mafunzo Yaliyotokana na Mradi wa Titye ...... 13
5.2 Uendelevu na Mikakati ya Mradi ...... 14
**SURA YA SITA ...... 15**
**HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ...... 15**
6.0 Hitimisho ...... 15
6.1 Mapendekezo ...... 15
**MAREJEO ...... 17**

**SHUKRANI**

Mradi huu unahusisha ushirikiano baina ya Mradi wa Uboreshaji Mazingira ya Biashara (LIC), Jumuiya ya Tawala za Mitaa (ALAT) na Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu (HWK). Mradi umefadhiliwa na Ubalozi wa Denmark kupitia mradi wa LIC uliopo nchini Tanzania.

Ninapenda kutumia fursa hii kutambua mchango muhimu wa kifedha kutoka kwa ubalozi wa Denmark uliofanikisha mradi wa Mradi wa Uboreshaji Mazingira ya Biashara (LIC) na ambao umefanikisha maandalizi ya ripoti hii. Shukrani za kipekee zimfikie mratibu wa mradi huu, Ndg. Flemming Winther Olsen na timu nzima ya mradi kwa msaada wao mkubwa uliowezesha kutekelezwa kwa mradi huu kwa kushirikiana na washirika wengine wa ndani kama vile Partners, OR-TAMISEMI, TNBC, TPSF na TCCIA.

Pia, ninatoa pongezi za dhati kwa serikali ya mkoa wa Kigoma, Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu na uongozi wa skimu ya Titye kwa kukubali kutoa taarifa muhimu zilizofanikisha uandishi wa ripoti hii.

Mwisho, ninapenda kuwashukuru sana ALAT, wafanyakazi wa OR-TAMISEMI, hasa Bi. Husna Kandoro, Bw. Vicent Chomola na Bw. Anicetus S. Mramba kwa kukusanya taarifa zilizowezesha uandishi wa ripoti hii.

Abdallah S. Ngodu
**Katibu Mkuu – ALAT**

# UTANGULIZI

Uandishi wa ripoti hii kuhusiana na Mradi wa Umwagiliaji wa Titye umewezeshwa na ALAT kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu chini ya ufadhili wa LIC. Mradi huu unaweza kutazamwa kama matokeo chanya katika kukabiliana na changamoto katika maeneo ya uzalishaji.

Changamoto kubwa zilizobainika katika mradi huu ni pamoja na mambo yafuatayo; hali ya upotevu mkubwa wa maji na ukosefu wa miundombinu imara ya ugawaji maji. Matengenezo hufanyika kwa lengo la kuimarisha mifumo ya ugawanyaji maji. Matengenezo haya yana lengo la kuimarisha upatikanaji wa maji hasa kipindi cha kiangazi ambacho kuna mahitaji makubwa ya umwagiliaji. Pia, mradi una lengo la kushajiisha, kuanzisha na kuimarisha chama rasmi cha wakulima. Chama hiki kitakuwa na majukumu rasmi ya kisheria ya kuendesha na kufanya matengenezo katika mradi. Baada ya matengenezo na maboresho ya mradi wa skimu ya Titye, tathmini ya upatikanaji wa chakula na hali ya umasikini itafanyika kwa ngazi ya familia.

Ripoti hii imesheheni data muhimu kutoka katika Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu. Pia, imejumuisha hali ya shughuli za kiuchumi, hali ya miundombinu na utayari wa wakulima katika kushiriki katika skimu. Ripoti hii ni muhimu sana kwa kuwa inatoa taarifa muhimu zinazoweza kutumiwa na watunga sera, watu wa mipango, watafiti na wahisani.

ALAT inaamini kuwa taarifa hizi ni muhimu kuzifikia Halmashauri nyingine zilizo nje ya Kasulu. Watu wote mnakaribishwa kwa maswali na maoni kuhusu andiko hili. Michango yenu ni muhimu sana na itatufaa katika kuboresha toleo lijalo la ripoti hii.

# VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| ALAT | Association of Local Authorities of Tanzania |
| DBCs | District Business Councils |
| DC | District Council |
| DIDF | District Irrigation Development Fund |
| HWK | Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu |
| LGA | Local Government Authorities |
| LIC | Local Investment Climate |
| Mha | Million Hectares |
| MoWI | Ministry of Water and Irrigation |
| NIDF | National Irrigation Development Fund |
| NIMP | National Irrigation Master Plan |
| NIRC | National Irrigation Commission |
| OsBC | One Stop Business Centre |
| O & M | Operation and Maintenance |
| OR-TAMISEMI | Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| SIFF | Small Industrial Facilitation Fund |
| TBS | Tanzania Bureaus of Standards |
| TCCIA | Tanzania Chamber of Commerce, Industries and Agriculture |
| TNBC | Tanzania National Business Council |
| ToT | Trainers of Trainees |
| TPSF | Tanzania Private Sector Foundation |

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.0. Usuli

Tanzania ipo katika nchi za Afrika Mashariki. Kwa upande wa Kaskazini inapakana na nchi ya Uganda na Kenya, wakati upande wa Magharibi inapakana na nchi ya Burundi, Rwanda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC). Upande wa Kusini, Tanzania inapakana na nchi ya Msumbiji, Malawi na Zambia, hali kadhalika upande wa Kaskazini Mashariki kuna mlima Kilimajaro na Magharibi kuna bahari ya Hindi.

Nchi hii ina ukubwa wa kilomita za mraba 947,300 na ina jumla ya mikoa 30. Kati ya hiyo, mikoa 25 iko Tanzania Bara na mikoa 5 ipo Zanzibar kama inavyooneshwa katika kielelezo hapo chini. Kulingana na sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012, Tanzania ina idadi ya watu zaidi ya milioni arobaini na nne.

Wilaya ya Kasulu ina eneo la kilomita za mraba 5,324 ambalo ni sawa na asilimia 10.62% ya eneo lote la mkoa wa Kigoma. Wilaya hii inapakana na nchi ya Burundi kwa upande wa Kaskazini na kwa upande wa Mashariki inapakana na wilaya ya Kibondo. Upande wa Kusini inapakana na wilaya ya Uvinza, upande wa Magharibi inapakana na wilaya ya Kigoma. Kwa upande wa Kaskazini Magharibi inapakana na wilaya ya Buhigwe. Kwa usafiri wa barabara, mji wa Kasulu upo umbali wa Km 78 (maili 48) kutoka Kigoma mjini ambako ndio makao makuu ya mkoa, upande wa Kaskazini Mashariki. Wilaya ya Kasulu ipo umbali wa Km 800 (maili 500) kutoka mji mkuu wa nchi, yaani Dodoma. Mji wa Kasulu upo nyuzi 4° 34' 48.00"S, 30° 6' 0.00"E (Latitudo: 4.5800; Longitudo: 30.1000). Kasulu ipo juu kwa mwinuko wa 1,100 mpaka 1,800 kutoka usawa wa bahari.

Shughuli kubwa ya kiuchumi nchini Tanzania ni kilimo ambacho huchangia asilimia 25% ya pato la ndani la taifa (GDP) na mapato ya nje ambayo ni 30.9%. Pia, kupitia shughuli za kilimo zimeajiri asilimia 70 ya wananchi wote wa Tanzania. Wilaya ya Kasulu ina eneo kubwa linaloweza kutumika kwa kilimo cha umwagiliaji. Eneo hilo linakadiriwa kuwa na hekta milioni 29.4. Kati ya hizo, hekta milioni 2.3 zinafaa kwa kilimo cha umwagiliaji. Eneo la uwanda wa wastani una eneo la hekta milioni 4.8 wakati eneo lililo kubwa lina hekta milioni 22.3 kwa ajili ya umwagiliaji pekee (Wizara ya Maji na Umwagiliaji, 2010).

Pamoja na kuwa na eneo kubwa na muhimu linaloweza kutumika kwa kilimo cha umwagiliaji, katika wilaya ya Kasulu, ni hekta 310,745 pekee ndizo zilizokuwa zimeendelezwa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji hadi kufikia mwaka 2009 (Wizara ya Maji na Umwagiliaji, 2010).

Wakulima wadogowadogo katika Tanzania ndio wanaoshughulika sana na kilimo cha umwagiliaji kwa kutumia umwagiliaji wa asili wa kutumia uchepushaji wa mito na maji ya mvua. Wengi wanatumia miundombinu duni ambayo huzalisha mazao hafifu. Kwa mfano, kuna miundo mbinu iliyo bora kwa umwagiliaji ambayo ingelifaa kuwa mfano na kuna ambayo ipo duni na inahitaji kuboreshwa (Bos, et al., 2005). Kwa upande mwingine, kilimo cha umwagiliaji tangu mwaka 1960– 1980 kimekuwa na changamoto kutokana na sababu mbalimbali, zikiwemo changamoto za kisera, matatizo ya kiufundi, mipango na hata usimamizi wake (Wizara ya Maji na Umwagiliaji, 2010).

Mnamo mwaka 1985 kilimo cha umwagiliaji kilipata msukumo mpya baada ya serikali na mashirika mbalimbali kutoka nje kuanza ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji na kuanzisha vikundi vilivyosajiliwa vya matumizi ya maji, mfano Jumuiya ya Watumiaji wa Maji (*Water Users Associations*) na Chama cha Wakulima wa Umwagiliaji (*Irrigators Organizations*) (Wizara ya Maji na Umwagiliaji, 2010).

Uimarishaji wa miundombinu ya umwagiliaji ulilenga kujenga miundombinu ya kudumu na kuleta vifaa vya kisasa vya umwagiliaji kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji. Ilitegemewa kuwa, kwa kuimarisha miundombinu hiyo kutaongeza matumizi bora ya maji na kuongeza mazao na kipato kwa mkulima.

Katika kutathmini ufanisi wa mradi wowote wa kilimo cha umwagiliaji, ni muhimu kufahamu mambo yanayochangia ufanisi wa miradi hii, mfano ukubwa wa mradi husika, shughuli yenyewe ya umwagiliaji, utawala wa mradi, upatikaji wa maji utoshelevu wa maji katika skimu husika na ushiriki na mchango wa wakulima katika uanzishwaji wa skimu (Inocencio, et al., 2005).

Kwa mujibu wa Makori (2005) kitendo cha serikali na mashirika ya kimataifa kushiriki moja kwa moja katika uimarishaji wa miundombinu ya asili ya skimu za umwagiliaji kulionesha uungaji mkono wa moja kwa moja wa miradi ya asili ya kilimo cha umwagiliji. Hivyo basi, kwa umuhimu huohuo ni wazi kuwa upo umuhimu LIC kufanikisha uimarishaji/ufufuaji wa mradi wa skimu ya umwagiliaji ya Titye.

### 1.1. Idadi ya Wakazi wa Wilaya ya Kasulu

Kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012, Wilaya ya Kasulu ina jumla ya idadi ya watu 425,794. Kati yao, 207,421 ni wanaume na 218,373 ni wanawake. Inakadiriwa kuwa, wilaya ina ongezeko la watu kwa 2.4% kila mwaka. Kwa mujibu wa taarifa za Halmashauri hii, ilikadiriwa kuwa, hadi kufikia mwaka 2017 idadi ya watu itaongezeka na kufikia watu 476,889. Katika ongezeko hilo wanaume ni 232,312 na wanawake ni 244,577.

### 1.2. Tatizo la Utafiti

Mradi wa umwagiliaji wa Titye hauna uimara kutokana na matumizi yasiyo sahihi na usambazaji mbovu wa maji. Hali hii imechangiwa na kuwepo kwa kilimo duni ambacho kwa ujumla wake kimesababisha upungufu wa mazao katika kijiji. Mfereji mkubwa uliochimbwa na wananchi unasababisha upungufu wa maji katika kijiji. Mfereji huu unavujisha maji mengi, hivyo, umesababisha upungufu wa maji kufika katika vitalu/mashamba. Kwa hali hiyo, umesababisha upungufu wa chakula katika ngazi ya kaya, kuongezeka umasikini, matatizo ya kiafya, maisha duni na uharibifu wa mazingira.



Kielelezo Na. 1: Hali ya mfereji wa Titye kabla ya kufanyiwa matengenezo. Hali hii ilisabibisha upotevu mkubwa wa maji na kusababisha uzalishaji duni wa mazao.

Skimu hii ya umwagiliaji ilianza rasmi mwaka 1982 kwa kupokea fedha kutoka Serikali Kuu pamoja na mashirika ya kimataifa yasiyo ya kiserikali. Hii ni kutokana na ukweli kuwa, shughuli za umwagiliaji zilikuwa chini ya Serikali Kuu. Mnamo mwaka 2014, wakati LIC ilipoanza utekelezaji wa mradi huu katika Wilaya ya Kasulu, walichangia katika kuboresha skimu ya umwagiliaji ya Titye kupitia fedha za mfuko uimarishaji viwanda vidogovidogo (SIFF). Kupitia fedha hizo walijenga miundombinu kwa ajili ya kumwagilia hekta 575, kuchimba mfereji mkubwa kwa km 5, kuchimba mifereji midogomidogo na ile ya kati, kuweka mipaka ya mashamba na kuunyoosha mfereji mkuu kwa mita 700.



Kielelezo Na. 2: Picha hii inaonesha hali ilivyo baada ya ujenzi katika chanzo cha maji kinachosambaza maji katika mradi.

Mnamo mwaka 2002 mradi ulishindwa kuendelea na kusimama kabisa kutokana na upungufu wa fedha. Hivyo basi, kutokana na hali hiyo, ni hekta 250 tu zilizoendelezwa tena kwa kiwango fulani tu. Baada ya mradi wa majaribio kuisha, kulisababisha maeneo mengine kukosa maji. Pia, baadhi ya maeneo, mifereji haikusawazishwa vilevile baadhi ya maeneo hapakuwa na vifaa vya kuzuia na kugawanyia maji. Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu ilijaribu kuufufua mradi huu mara mbili bila mafanikio hata pale walipopatiwa fedha kutoka Serikali Kuu.



Kielelezo Na. 3: Picha ya upande wa kushoto inaonesha ujenzi wa mfereji ulipoishia na ile ya kulia inaonesha mkulima akiwa amebeba mazao yake yanayotokana na skimu ya umwagiliaji.

Kutoka na maelezo yote yaliyotolewa hapo juu, LIC kwa kushirikiana na ALAT na Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, kwa pamoja, waliamua kushirikiana kufufua skimu ya umwagiliaji ya Titye ili kuzitatatua changamoto zilizobainishwa.

## 1.3. Eneo la Mradi

Mradi wa umwagiliaji wa Titye upo katika kijiji cha Titye, kata ya Titye katika Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu. Skimu hii ipo umbali wa Km 32 kutoka Kasulu mjini. Skimu hii ilianzishwa mwaka 1982 ikiwa kama mradi wa majaribio kwa ajili ya kilimo cha mpunga chini ya serikali ya Tanzania kwa msaada wa serikali ya watu wa Japan. Uanzishwaji wa mradi huu ulikadiriwa kutumia Tsh milioni 100. Lengo la mradi lilikuwa kuongeza mavuno na mapato kwa mkulima na pia kumwezesha mkulima kulima mara mbili kwa mwaka. Mradi ulitekelezwa chini ya usimamizi wa serikali ya mkoa wa Kigoma kwa usimamizi wa kiufundi kutoka Idara ya Umwagiliaji, kanda ya Tabora.

Mradi huu una eneo la hekta 575. Hata hivyo, chini ya mradi wa majaribio ni hekta 250 tu zilizoendelezwa tena zikiwa hazijakamilika vizuri kwa baadhi ya maeneo. Kutokamilika kwa mradi kumechangia mradi kutofikia malengo yake, yaani kuongeza uzalishaji wa mazao kwa wakulima. Hata hivyo, wanakijiji wa Titye wanautumia mradi huu kuzalisha mpunga na wameungana na kuanzisha kikundi ambacho mwaka 2012 kilisajiliwa kwa nambari S.A.18400 chini ya kifungu cha sheria ACT. Cap. 337 RE cha mwaka 2002. Kikundi hicho kinajulikana kwa jina la UWAMPUTI (Umoja wa Wakulima wa Mpunga Titye). Kikundi cha UWAMPUTI kina jumla ya wanachama 720. Pia, kuna bodi inayowaongoza wanachama ambayo inasimamia mambo yote yanayohusiana na skimu. Lengo kuu la kikundi ni kuwahamasisha na kuwasaidia wakulima kuongeza uzalishaji.



Kielelezo Na. 4: Ramani (Mchoro) ya Mradi wa Titye.

### 1.4. Malengo

#### 1.4.1. Lengo Kuu

Lengo kuu la mradi lilikuwa ni kuongeza ufanisi katika matumizi ya maji kwa kupunguza upotevu wa maji na kutumia mbinu mpya za umwagiliaji wa kisasa. Pia, kuimarisha ushirikiano wa wadau wote katika shughuli za umwagiliaji kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa skimu na utawala wake.

#### 1.4.2. Malengo Mahususi

Kwa umahususi kabisa mradi ulilenga usimamizi na tathmini katika maeneo yafuatayo**:**

1) Ukarabati wa miundombinu hasa mifereji ya kupitisha maji, mifumo ya kudhibiti maji, na njia za kuingia katika mashamba;
2) Kuwajengea uwezo wanufaika wa mradi;
3) Kuwezesha uwekezaji katika mnyororo wa thamani katika kilimo; na
4) Kuhimiza uzalishaji wa mpunga kwa kutumia mbegu bora.

### 1.5. Eneo la Mradi

Wakulima wengi katika wilaya ya Kasulu hutegemea mvua na kilimo cha umwagiliaji ambacho kwa kawaida hutokana na maji ya mvua au maji ya mito. Wengi wa wakulima hawa wanajihusisha na kilimo cha mpunga kama zao la chakula na biashara. Wakulima wa skimu ya umwagiliaji ya Titye kwa kiasi kikubwa hutegemea maji ya mto kwa ajili ya kumwagilia mazao yao. Hivyo basi, mradi huu ulilenga kukarabati miundombinu, kuongeza mnyororo wa thamani katika kilimo na kuongeza uzalishaji katika skimu husika.

## SURA YA PILI
## UFUMBUZI WA MATATIZO

### 2.1 Mfereji wa Umwagiliaji

Maji ya umwagiliaji hupatikana kutokana na mifereji ambayo ilikwisha andaliwa kutoka mfereji mkubwa na mifereji midogomidogo. Mara nyingi mifereji hiyo kuta zake huwa siyo imara, na ina miteremko isiyo sawa. Hali hii husababisha kasi ya maji kupungua, kuongezeka kwa matope katika mifereji na upotevu mkubwa wa maji.

Aidha, mradi ulikuwa na ukubwa wa hekta 575. Kwa msaada wa LIC umefanikiwa kuendeleza hekta 250 kwa kukarabati na kujenga upya mfereji wenye urefu wa mita 2,349 na upana wa mita 545. Ujenzi huu ulikuwa ni muhimu ili kuongezea ufanisi wa mfereji wa umwagiliaji, kuongeza ufanisi katika matumizi ya maji na utawala bora.

### 2.2 Uendeshaji na Ukarabati

Kulingana na mahojiano yaliyofanyika katika eneo la mradi, iligundulika kuwa uendeshaji na ukarabati wa miundombinu ya mradi hufanywa na wakulima wenyewe kabla ya kuanza kwa msimu au/na mwishoni mwa msimu. Miongoni mwa shughuli walizofanya wakulima ni pamoja na usafishaji wa mifereji kwa kuondoa magugu na urekebishaji wa kuta ili kuzuia upotevu wa maji usio wa lazima. Aidha, pale ilipohitajika ukarabati au matengenezo makubwa kwa kawaida shughuli hii hufanywa kwa kushirikiana na serikali ya wilaya kupitia idara husika.

Katika msimu wote wa kilimo, mara nyingi ukarabati mdogomdogo hufanywa na wakulima wenyewe katika maeneo yao jambo ambalo kwa kiasi fulani huleta changamoto kwa kuwa sio maeneo yote yanayosafishwa na kukarabatiwa kwa ubora unaolingana na kwa wakati.

Kulingana na taratibu zilizowekwa na chama cha wakulima katika skimu hii, kila mkulima hutakiwa kutenga kilo 40 za mpunga kama mchango wake kwa uendeshaji na ukarabati wa mradi.

### 2.3 Usambazaji wa Maji na Mifumo ya Udhibiti

Hapakuwa na mifumo ya kisasa ya kusambazia maji katika skimu hii. Mwanzo kabisa, udhibiti na usambazaji wa maji ulifanyika kwa kutumia mifumo isiyofaa na ya kizamani hali iliyochangia kuwepo kwa ufanisi duni katika skimu. Hivyo, mradi ulilenga kufanya yafuatayo: Utengenezaji wa mifumo ya kitaalamu ya kusambazia maji kama vile milango mitatu ya kukinga maji, maboksi kumi ya kugawanyia maji, maeneo mawili ya kushushia

maji na madaraja 11 yanayozunguka mradi. Haya ni baadhi ya mahitaji yaliyokuwa yanahitajika ili mradi uendeshwe kisasa.

## 2.4 Uwezeshaji wa Wakulima na Shughuli Nyingine katika Mradi

Wakulima waliwezeshwa ili waweze kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa mradi kwa kusaidiwa kuanzisha chama chao kilichosimamia shughuli za usambazaji wa maji, uendeshaji na ukarabati wa miundo mbinu ya skimu. Pia, walipatiwa mafunzo mbalimbali ambayo yalifanya watambue kuwa mradi ulikuwa wao na kuwafanya waupende kwa kuuhudumia ipasavyo kwa manufaa yao na mradi husika. Ili kufikia malengo ya uzalishaji bora, wakulima walipewa mafunzo kuhusu mambo yafuatayo:

1) Namna ya kuchagua mbegu bora;
2) Uzalishaji bora kwa kutumia mbolea na matumizi bora ya ardhi;
3) Matumizi sahihi na uhifadhi wa rasimali ya maji;
4) Upandaji mpunga kwa kutumia nafasi stahiki;
5) Kilimo-kibiashara na utafutaji wa masoko;
6) Utunzaji na uhifadhi wa mazingira; na
7) Namna ya kuongeza mnyororo wa thamani katika mazao ya biashara.

Ilipangwa kuwa mambo haya yatolewe kupitia mafunzo yaliyopo katika mpango na mtiririko maalumu.

## 2.5 Usimamizi wa Kazi

ALAT, Kamisheni ya Umwagiliaji ya Taifa (*National Irrigation Commission*) kanda ya Tabora kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, walisimamia mradi huu kwa kuandaa michoro, kufanya usanifu na kusimamia mkataba wa mradi.

# SURA YA TATU

# UTEKELEZAJI, MPANGILIO NA MATOKEO/ MATARAJIO YA MRADI

## 3.1 Utekelezaji na Majukumu yao

Mtekelezaji mkuu wa mradi huu ni ALAT akishirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu, Kamisheni ya Taifa ya Umwagiliaji Kanda ya Tabora. Kamisheni ya Taifa ya Umwagiliaji Kanda ya Tabora na washirika wengine walikuwa na jukumu la kuhakikisha kuwa mradi unatekelezwa kama ulivyopangwa. Kwa ujumla, wao walihusika na upembuzi yakinifu, michoro, umwagiliaji, uchimbaji wa mifereji na usimamizi wa mradi kwa pamoja. Michoro ya miradi iliandaliwa na Kamisheni ya Umwagiliaji, kanda ya Tabora ambayo pia ilihusika na ukarabati na ujenzi wa mradi.

Aidha, Kamisheni ya Taifa ya Umwagiliaji Kanda ya Tabora ilihusika katika uandaaji wa BOQ na utoaji wa zabuni kwa kuhusisha Kamati ya Zabuni ya Wilaya.

## 3.2 Ushiriki wa LIC na Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu Kwenye Mradi wa Umwagiliaji wa Titye

Maombi ya fedha kutoka katika Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu kwa ajili ya mradi yalipokelewa Disemba 2014. Halmashauri ilikadiria kuwa walihitaji Tsh. 750,213,250/= kwa ajili ya kumalizia hekta 250 za skimu ya umwagiliaji. Pia, walihitaji Tsh. 500,000,000/= kama mtaji kwa wakulima kutoka benki za biashara. Aidha, walikadiria kuwa zilihitajika Tsh. 250,213,250/= kama ziada, na kuwa fedha hizi zingepatikana kutoka katika Halmshauri na wanachama na kufanya jumla kuu kuwa Tsh. 750,213,250/=.

Mnamo Aprili 2015, LIC walikamilisha mazungumzo na shirika la kilimo binafsi– Private Agricutural Sector Support (PASS) na ilipofikia 31/07/2015 mazungumzo yalionesha mradi ungeliweza kuleta faida kama utaanza. Mpaka ilipofika 23/05/2016 mpango kazi ulipitishwa mpango kazi huu ulionesha kuwa mradi ungeliweza kuleta faida ya Tsh. 62,848,083/= katika mwaka wa kwanza, baada ya kuuza MT 1,438 za mpunga kwa bei ya Tsh. 667,000/= kwa tawi moja, au Tsh. 667/= kwa kilo moja au Tsh. 43,355/= kwa gunia la kilo 65. Mradi ulitarajia kupata mapato ya Tsh. 1,859,516,551/=.




Kielelezo Na. 5: Kikao cha kuthibitisha Mpango Kazi

Utafiti ulionesha mradi unaweza kujiendesha hivyo LIC ilikubali kuwapa msaada wa fedha Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu kama walivyoomba ili waweze kuendesha mradi wa hekta 250 kwa kuanzia.

Mnamo tarehe 8 Juni, 2016 Bodi ya Zabuni ya Wilaya iliichagua kampuni ya Western Constuction Co. Ltd kumalizia skimu hii. Na mnamo tarehe 30 Juni, 2016 mkataba ulisainiwa ili kuianza kazi ya ujenzi ambayo hadi sasa inaendelea.

## 3.3 Matarajio ya Mradi

### 3.3.1 Kuongeza Uzalishaji wa Mazao, Kipato cha Mkulima na Kupunguza Umasikini

1. Kwa kuongeza upatikanaji wa maji na ukulima wa kisasa mazao yataongezeka;
2. Itasaidia kuboresha hali za maisha na huduma mbalimbali za kijamii vijijini na kutawavuta watu wengi katika kilimo, hivyo basi, itawahamasisha vijana kubaki vijijini na kujihusisha na kilimo; na
3. Kwa kuwashirikisha wakulima katika mradi wa umwagiliji itakuwa ni sehemu ya utekelezaji wa ahadi ya serikali ya kuimarisha maisha ya watu na kupiga vita umasikini hasa katika maeneo ya vijijini.

### 3.3.2 Uimarishaji Matumizi ya Maji katika Skimu

1) Uimarishaji wa mifumo ya skimu iliyopo;

2) Uimarishaji wa matumizi ya maji na kupunguza upotevu wa maji;

3) Wakulima kutumia njia za kisasa za umwagiliaji na hivyo kuimarisha matumizi sahihi ya maji; na

4) Ongezeko la matumizi sahihi ya ardhi.

### 3.3.3 Kuwajengea Uwezo Jumuiya ya Umwagiliaji

Wakulima walihamasishwa na kufanikiwa kuanzisha jumuiya yao ili watambulika kisheria. Lengo la jumuiya hii ilikuwa ni kusimamia masuala yote ya ndani yanayohusiana na skimu. Jumuiya hii inao viongozi wake kama vile Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Katibu, Mhasibu na wajumbe 5 wa bodi. Pia, jumuiya inazo kamati 4 za umwagiliaji; Kamati ya Kilimo na Mazingira, Kamati ya Uendeshaji na Ukarabati/ Matengenezo, Kamati ya Utawala, Kamati ya Mipango, Kamati ya Uchumi na Fedha, Kamati ya Utatuzi na wanachama wenyewe. Mradi una jumla ya wanachama 720, kati yao 497 ni wanaume na 223 wanawake.



Kielelezo Na 6: Viongozi wa skimu ya Titye wakiwa katika moja ya kikao rasmi cha mradi.

## SURA YA NNE

## GHARAMA NA UPATIKANAJI WA FEDHA ZA KUENDESHA MRADI

### 4.1 Gharama za Mradi

Gharama za mradi zinajumuisha fedha za kujenga miundombinu ya skimu na gharama za kuwajengea uwezo wanachama wa skimu hii. Gharama zote za mradi zilikadiriwa kuwa Tsh. milioni 790. Gharama hizi zilijumuisha pamoja na gharama za usimamizi Tsh 15,484,000/=. katika gharama hizi Mradi wa Uboreshaji Mazingira ya Biashara (LIC) walichangia Tsh. milioni 790, wilaya ya Kasulu waliutoa mchango wa kiufundi na wananchi walijitolea nguvu zao katika uendeshaji na ukarabati wa miundombinu.

### 4.2 Muda wa Utekelezaji wa Mradi

Gharama za mradi huu ilikadiriwa ni miezi 6 na siku 15, kuanzia tarehe 30/06/2016 na kumalizika tarehe 11/01/2017 kwa mujibu wa kalenda.

## SURA YA TANO

## CHANGAMOTO, VIKWAZO NA UIMARA WA MRADI

### 5.0 Changamoto

i. Kusawazisha baadhi ya maeneo katika skimu, LIC wamekubali kusawazisha maeneo hayo baada tu ya wakulima kung'oa michikichi iliyopo;
ii. Wakulima wamekosa soko la uhakika katika mkoa kwa ajili ya kuuza mazao yao. Aidha, mazao mengi huuzwa ndani ya wilaya kwa bei ambayo hupangwa na madalali;
iii. Kutokuwepo na maghala ya kuhifadhia mazao yanayotokana na mradi. Kwa hali hii, hata ile asilimia 5 ambayo ilikubaliwa kuwa itengwe kwa shughuli za ukarabati hakuna mahali pa kuiweka;
iv. Kutokamilika kwa uchimbaji wa mifereji ya skimu kwa wakati muafaka;
v. Kukosekana kwa fedha za utafiti wa udongo wenye lengo la kubaini dawa inayofaa ya kuzuia wadudu waharibifu; na
vi. Ukosefu wa rasilimaliwatu hasa maafisa kilimo kwa ajili ya usimamizi wa shughuli zote za kilimo katika skimu. Kutokana na hali hii, wakulima wengi wameendelea kutumia mbegu za kizamani hali inayochangia mapato duni.

### 5.1 Mafunzo Yaliyotokana na Mradi wa Titye

i. Ushirikishwaji wa wananchi katika usimamizi na ukarabati wa mradi ulitoa hamasa kubwa kwa wananchi. Pia, katika utekelezaji wa mradi, mchango wa kilo 40 za mpunga kwa ajili ya akiba ya usimamizi na ukarabati ulileta hamasa kubwa kwa wakulima na kuona kuwa mradi ni wao;
ii. Uimarishaji wa miundombinu ya skimu kuliongeza upatikaji wa maji kwa wingi. Hali hii ilichangia ongezeko la mavuno na kubadili hali ya maisha kwa kupunguza wimbi la umasikini katika eneo la mradi; na
iii. Kuongezeka kwa mavuno ya mpunga, utafiti umeonyesha kuwa kuwa kuna ongezeko kubwa la mavuno katika skimu baada ya ukarabati wa miundombinu. Kabla ya ukarabati, wakulima walikuwa wakivuna magunia 19 kwa hekta na baada ya ukarabati mavuno yaliongezeka na kufika magunia 40 kwa hekta. Mafanikio haya ni ushahidi kuwa mbegu bora ziliongeza tija kwa wakulima na kwamba mradi ulikuwa na faida.

Ni muhimu kutaja kuwa, mafunzo yaliyotokana na mradi huu ni ushahidi unaojitosheleza kuwa miradi ya umwahiliaji inaweza kuleta tija kama itasimamiwa vizuri.

## 5.2 Uendelevu na Mikakati ya Mradi

Kama ilivyotajwa huko nyuma, Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu kwa kushirikiana na viongozi wa wakulima na wakulima wenyewe wamekubaliana kushirikiana kwa pamoja katika uendeshaji wa skimu kwa kuchangia kg 40 za mazao kila mwaka. Aidha, wamekubalina kufanya chaguzi za viongozi wa skimu kwa wakati kama katiba ya chama inavyosema. Pia, wamekubaliana kushirikiana kuondoa migogoro inayohusiana na matumizi ya maji kwa kuzingatia miongozo na taratibu walizokubaliana.

# SURA YA SITA
# HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 6.0 Hitimisho

Ripoti hii imebainisha mikakati inayoweza kutumika katika utekelezaji wa miradi ya kijamii ya umwagiliji. Msaada wa serikali na mashrika ya kimataifa ni muhimu sana katika kuifanikisha miradi hii. Imedhihirika wazi katika mradi wa skimu wa Titye kuwa, ushiriki wa wananchi kwa kutumia nguvu zao, kuwepo kwa vyama/ vikundi rasmi vilivyosajiliwa, matumizi bora ya maji, upatikanaji wa maji ya uhakika, ukulima wa kisasa n.k ni sehemu muhimu katika mafanikio ya miradi ya umwagiliji.

Pia, miradi ya umwagiliaji inayojumuisha jamii ikisimamiwa vizuri inaweza kuleta tija na kuweza kuwa mkombozi wa kupunguza wimbi la umasikini katika jamii, kama ilivyoonyesha katika mradi wa umwagiliaji wa Titye katika Wilaya ya Kasulu. Hivyo basi, serikali na wadau wengine hasa wafadhili wanaweza kutumia uzoefu wa mradi wa umwagiliji wa Titye kama mfano katika wilaya na mikoa mingine.

## 6.1 Mapendekezo

Mapendekezo haya yametolewa kulingana na utafiti uliofanywa katika mradi wa Titye kwa lengo la kuboresha ufanisi wa mradi. Pia, yamezingatia changamoto zilizojitokeza katika mradi kutokana na upungufu wa fedha. Hivyo basi, mapendekezo ya ripoti hii ni haya yafuatayo:

i. Kuendelea kuwashirikisha wananchi katika usimamizi/ uendeshaji na ukarabati wa miundombinu ya mradi;
ii. Kuendeleza utafiti wa mbegu za mpunga za kisasa ambazo zinaweza kuleta tija kubwa kwa wakulima;
iii. Kuongeza mavuno ya mpunga kwa kutumia kilimo cha mzunguko katika sehemu ya msimu. Mfano, kupanda mazao mengine kama vile maharage kwa lengo la kuongeza rutuba katika udongo;
iv. Kufanyika utafiti wa udongo wa mara kwa mara ili kutathmini ubora wa udongo kwa shughuli za umwagiliaji;
v. Serikali na wadau wengine wasaidie upatikaji wa masoko ya mpunga ya uhakika kwa lengo la kuinua kipato cha wakulima wadogo;
vi. Wakulima wengi wana uwezo mdogo wa kifedha, hivyo ni muhimu kwa serikali na wadau wengine kuwasaidia namna rahisi ya kupata mikopo katika taasisi za fedha;

vii. Wakulima wafundishwe njia bora za kuhifadhi kumbukumbu;

viii. Wakulima wafundishwe kuhusu athari za tabianchi na namna ya kukabiliana nazo ili zisiathiri kilimo chao; na

ix. Serikali na wadau wengine wanatakiwa kuongeza nguvu kwa kusaidia miradi ya umwagiliaji kama hii. Ni muhimu wakatambua kuwa miradi hii inachangia upatikanaji wa chakula na kuondosha umasikini katika ngazi ya kaya hasa katika maeneo ya vijijini. Miradi ya kupigiwa mfano kama hii ni muhimu ikaigwa na kujengwa katika wilaya na mikoa mbalimbali kwa lengo la kuchochea maendeleo katika maeneo hayo.

## MAREJEO


Bos MG, Burton MA, Molden DJ (2005): Irrigation and drainage performance assessment: Practical guideline.

Inocencio A, Kikuchi M, Merrey D, Tonosaki M, Maruyama A, de Jong I, Sally H, Vries Pd (2005): Lessons from Irrigation investment experiences: Cost-reducing and performance enhancing options for Sub-Sahara Africa. International Water Management Institute.

Makori GM (2015): Permance evaluation of traditional and and irrigation schemes in Tanzania – A case study of three irrigation schemes in Mvomero District Council, Morogoro Region.

MoWI (2010): The National irrigation Policy, Ministry of Water and Irrigation. The United Republic of Tanzania.

World Bank (2004): River Basin Management and Smallholder Irrigation Improvement Project. Report No. 30929.

World Bank (2008): Agriculture for Development. World development report.

Kwa mawasiliano zaidi wasiliana na
Katibu Mkuu Mtendaji wa ALAT
S. L. P. 2049
Simu: +255 784 514 245
Dodoma, Tanzania
Barua pepe: info@alat.or.tz
Tovuti: www.alat.or.tz